## 6.0 Jinsi ya Ukamataji

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Sura ya 20, mtu atakamatwa na polisi au na mtu mwingine kwa kitendo cha kumgusa bega, mkono au kwa kumzuia kuondoka kwenda sehemu anayotaka.

Sheria inakataza kutumia nguvu za ziada wakati wa ukamataji na nguvu ya ziada itaumika tu iwapo mtuhumiwa anakataa kukamatwa kihalali. Sheria inalekeza kuepuka matumizi ya nguvu kupita kiasi.

## 7.0 Haki za Mtuhumiwa Wakati wa Ukamataji

- Kumtaka mtu anayemkamata ajitambulishe kwa jina, cheo, sehemu anayofanyia kazi;
- Kuelezewa sababu ya kukamatwa kwake;
- Kutoteswa, kupigwa kufanyiwa unyanyasaji wa aina yeyote, au kuwekwa kwenye mazingira au hali ngumu zaidi ili kumzuia asitoroke wakati ametii amri;
- Kuwasiliana na ndugu, jamaa au mwanasheria wake kuhusu kukamatwa kwake;
- Kufikishwa katika kituo cha polisi chochote kilichokuwa karibu yake au mahakamani ndani ya saa 24 tangu akamatwe ili taratibu nyingine za kisheria ziendelee. Iwapo amekamatwa na mtu binafsi anatakiwa akabidhiwe kwa Askari Polisi, au afikishwe katika kituo cha polisi kilicho karibu nae, kwenye ofisi za Kijiji au Kata za eneo ambalo amemkamata mtuhumiwa kwa ajili ya kuwekwa katika sehemu salama kabla ya kufikishwa kituo cha polisi;
- Kutonyang'anywa mali zake halali wakati wa kukamatwa au baada ya kukamatwa;
- Kupatiwa mahitaji yake muhimu kama chakula, malazi, na matibabu;
- Haki ya kutochukuliwa kama ana hatia hadi atakapotiwa hatiani na Mahakama yenye Mamlaka;
- Haki ya Kupata dhamana atakapofikishwa kituo cha polisi, iwapo kosa lake linadhaminika na amekidhi vigezo.

## 8.0 Wajibu wa Mtuhumiwa Wakati wa Kukamatwa

- Kutii amri halali ya polisi wakati wa kukamatwa;
- Kujibu maswali atakayoulizwa na polisi au mtu yeyote anayemkamata;
- Kutoa ushirikiano kwa chombo chochote kinachomkamata.

## 9.0 HITIMISHO

Mfumo wa haki jinai unaongozwa na taratibu, kanuni na sheria mbalimbali , hivyo basi ni vyema raia wakajua haki na wajibu wao ili kusaidia vyombo vya utekelezaji wa sheria ikiwemo Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya, na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

---

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# TARATIBU ZA UKAMATAJI

## TARATIBU ZA UKAMATAJI

### 1.1 Utangulizi

Tume. Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa.

Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

### 2.0 Maana ya Ukamataji

Ni kitendo cha kusitisha uhuru wa mtu kwa muda kwa kumuweka chini ya ulinzi wa vyombo vya utekelezaji wa sheria kwa lengo la kupisha upelelezi wa tuhuma zinazomkabili au kumuhifadhi kwa muda kwa ajili ya usalama wake. Ukamataji huweza kutekelezwa na vyombo vya utekelezaji wa sheria mathalani Jeshi la polisi, Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Askari polisi anatakiwa baada ya ukamataji,amfikishe mtuhumiwa kituo cha polisi kwa hatua nyingine za kisheria ikiwemo kupelekwa mahakamani ndani ya saa 24 tangu kukamatwa kwake.

Iwapo mtu binafsi amemkamata mtuhumiwa anatakiwa amkabidhi kwa askari polisi, au amfikishe katika kituo cha polisi kilicho karibu mara tuu baada ya kumkamata, au katika ofisi za kijiji au kata kwa ajili ya kuwekwa katika sehemu salama kabla ya kufikishwa kituo cha polisi.

### 3.0 Sheria Zinazosimamia Masuala ya Ukamataji

Sheria kuu inayoratibu uendeshaji wa makosa ya jinai nchini ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, ambayo pia inaainisha taratibu za ukamataji.

Vile vile kuna sheria nyingine kama Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa(Sura ya 200), Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura ya 95), Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Sura ya 329), Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori

(Sura ya 283), Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu (Sura ya 423) na sheria nyinginezo zinazohusika na ukamataji.

### 4.0 Mamlaka za Ukamataji

Sheria mbalimbali zimetoa mamlaka kwa watu waliyo ruhusiwa kisheria kukamata. Kwa mujibu wa sheria wafuatao ndio wenye mamlaka ya ukamataji;-

- **Maafisa kutoka vyombo vya utekelezaji wa sheria kama askari polisi, askari wanyamapori, maafisa uchunguzi;**
- **Hakimu**
- **Mgambo na Sungusungu**
- **Mtu binafsi (Atakamata iwapo tendo la uhalifu limefanyika mbele yake)**

### 5.0 Aina za Ukamataji

### 5.1Kumkamata Mshtakiwa bila Hati ya Kukamata

Ukamataji huu unaweza kutekelezwa na askari polisi au mtu yeyote katika mazingira yafuatayo;

i. Mtu atakayefanya tendo la uvunjifu wa amani mbele ya askari;
ii. Mtu anayemzuia askari polisi kufanya kazi zake, au atafanya jaribio la kutoroka au atatoroka kutoka chini ya ulinzi;
iii. Mtu atakayeonekana kuwa na mali ya wizi au inayoshukiwa kuwa ya wizi;
iv. Mtu yeyote ambaye amefanya kosa nje ya Tanzania na kuna uwezekano wa kuadhibiwa ndani ya Tanzania,
v. Mtu anayedharau nembo ya taifa kama vile wimbo wa Taifa au Bendera ya Taifa;
vi. Mzururaji au mtu anayezurura kwa nia ya kufanya uhalifu, mtu anayeshukiwa kuwa hati ya kukamatwa imeshatolewa dhidi yake.

### 5.1.2 Makosa Yasiyohitaji Hati ya Ukamataji

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 imeainisha makosa mengine ya jinai yasiyohitaji Hati ya Ukamataji bila kujali mazingira ya utendekaji wa kosa. Baadhi ya makosa haya ni;

- **Uhaini,**
- **Kuhamasisha uasi,**
- **Uharamia,**
- **Ugaidi,**
- **Kuandamana bila kibali,**
- **Kutumia lugha ya matusi na kupigana,**
- **Kuharibu ushahidi,**
- **Kusaidia wafungwa kutoroka,**
- **Ubakaji na kujaribu kubaka**
- **Shambulio la aibu,**
- **Kuendesha danguro ,**
- **Kulawiti na kujaribu kulawiti**
- **Wizi wa mtoto,**
- **Ukatili dhidi ya mtoto,**
- **Utapeli na uzururaji,**
- **Mauaji**
- **Kupatikana na viungo vya binadamu n.k**

### 5.2 Ukamataji kwa Kutumia Hati ya Kukamata

Ukamataji huu unafanyika katika namna mbili, ya kwanza ni pale ambapo mtuhumiwa atakuwa ameshafunguliwa mashtaka, na mahakama itamuita kwa kutumia hati ya kumkamata mtuhumiwa huyo na kama atakuwa hajafunguliwa mashtaka kabla hajakamatwa, basi wito utatumika kumtaarifu.

Aidha, sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 imeainisha baadhi ya makosa yanayohitaji hati ya ukamataji kama yafuatayo; Matumizi mabaya ya mamlaka, shambulio la kawaida, kusababishia hasara ya fedha au mali ya mamlaka fulani,tamko la uwongo ili kujipatia hati ya kusafiria, kuharibu noti za benki, kupuuza kuzuia kosa, uandikishaji askari wa kivita katika nchi za kigeni, kutishia, kutishia kuwajeruhi watumishi walioajiriwa katika utumishi wa umma, na kutelekeza watoto.